

MUNGU AMEPAA.

Zaburi Sherehe ya Kupaa Bwana

PETER AMMI
KIBOSHO SEMINARI
21 May 2022

$\text{♩} = 65$

Mu ngu a me pa a kwa ke le le za shangwe, Bwa na

kwa sa u ti ya ba ra gu mu.

1. Enyi watu wote pigeni makofi, mpigieni Mungu kelele kwa sauti ya shangwe/
Kwa kuwa Bwana aliye juu mwenye kuogofya; Ndiye Mfalme mkuu juu ya dunia yote.
2. Mungu amepaa kwa kelele za shangwe, Bwana kwa sauti ya baragumu/
Mwimbieni Mungu, naam, imbeni; Mwimbieni Mfalme wetu, naam, imbeni.
3. Maana Mungu ndiye Mfalme wa dunia yote, imbeni kwa akili/
Mungu awamiliki mataifa; Mungu ameketi katika kiti chake kitakatifu.